# esha fursa a Afrika

bayana katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26 wenye lengo la kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu.

Aliongeza kuwa benki inatumia fursa ya uimarishaji wa mifumo ya sheria na ya kitaasisi iliyofanywa na serikali hususan Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kwa lengo la kuboresha usimamizi na uratibu pamoja na mfumo wa kitaasisi kwa ajili ya uratibu wa programu ya ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi.

"Tunaishukuru serikali kwa kuonyesha nia na utayari wa kutuongezea mtaji, hali inayotupa fursa ya kutimiza malengo makubwa zaidi. Kutokana na kuwapo mazingira haya wezeshi ya kimtaji, benki itaendelea kuchangamkia fursa za maombi ya mikopo kutoka sekta za umma na binafsi hasa ile miradi ya maendeleo inayokidhi vigezo vya njia ya ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi na kuendana na ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi," alisema.

Mkataba wa Uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara la Afrika yaani uliridhiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Septemba 2021.



ca Tanzania, Adam Mihayo (wa pili kulia), kikao cha bajeti mwishoni mwa wiki.
CHA WETU

# neema wateja

za huduma zake kote nchini na kufungua maduka maalum ya Airtel Money zaidi ya 3,500 na wakala zaidi ya 2,000 huku ikiendelea kuwekeza katika kupanua mtandao wa 4G kwa minara yake yote na kuwafikia Watanzania wote hasa wanaoishi maeneo ya vijijini," alisema Ngululu.

Akipokea zawadi yake ya televisioni, Mkazi wa Dodoma, Thabiti Hemedi, aliishukuru Airtel kwa zawadi hiyo japo hakuitarajia, hivyo akawataka wateja wengine 'kuupiga mwingi' ili washinde zawadi kama yake kwa kuwa zawadi zinatolewa 'bila mchongo'.

Mshindi mwingine aliyejinyakulia jokofu, Silvano Chigwaye, alisema zawadi zote zinazotolea na kampuni hiyo kupitia promosheni zake ni za kweli na hakuna upendeleo.

# Wasaka mbinu za kuimarisha huduma

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI ya ufundi ya serikali mtandao imefanya kikao cha kwanza kujadili namna ya utekelezaji wa majukumu yake ili kuhakikisha jitihada za serikali mtandao zinaimarika na kuleta tija kwa umma.

Kikao hicho kilifanyika juzi katika Ofisi za Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) jijini Dodoma, kikiongozwa na Kaimu Mwenyekiti, Eric Kitali, Mkurugenzi wa TEHAMA Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Eric alisema kamati hiyo ipo kwa mujibu wa kifungu Na. 17 cha Sheria ya Serikali Mtandao ya Mwaka 2019, ambapo miongoni mwa majukumu yake ni kutoa ushauri wa kitaalamu, ili kuhakikisha utekelezaji wa Serikali Mtandao unakuwa ni wenye tija na kuongeza ufanisi katika utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa umma.

Alisema kamati ina wajumbe wachache kulinganishwa na idadi ya wizara na taasisi za serikali na kuwasihi wajumbe kutenda haki kwa kuwajibika na kuhakikisha wanatoa ushauri wenye tija katika eneo la TEHAMA ili kuhakikisha serikali mtandao inaimarika na kuleta tija.

"Ikiwa kamati hii itafanikiwa kuifanya mifumo ya TEHAMA katika taasisi za umma izungumze tutakuwa tumeisaidia sana serikali, kwani itaokoa rasilimali fedha na rasilimali watu," alisisitiza.

Katibu wa Kamati hiyo, Sylvani Shayo ambaye ni Mkurugenzi wa Udhibiti na Usalama wa TEHAMA e-GA alimtaja baadhi ya majukumu ya kamati hiyo kwa mujibu wa kifungu Na. 17(4) cha Sheria ya Serikali Mtandao ya mwaka 2019.

Majukumu hayo aliyataja kuwa ni; kupitia na kutoa mapendekezo juu ya Sera ya Serikali Mtandao itakayotekelezwa katika taasisi za umma, kupitia na kutoa mapendekezo juu mpango mkuu wa serikali mtandao na mkakati wake utakaotekelezwa na taasisi zote za umma.

"Kamati pia kupitia na kutoa mapendekezo juu ya miradi na programu za kitaifa za serikali mtandao na kutoa miongozo ya kiufundi katika kutatua migogoro kwenye utekelezaji wa miradi mikubwa ya TEHAMA katika taasisi za umma," alisema.

Majukumu mengine aliyataja ni kuishauri kamati ya kitaifa ya serikali mtandao kuhusu masuala ya serikali mtandao, kuandaa ripoti za robo mwaka na kuziwasilisha katika kamati hiyo.

Kamati hiyo iliazimia kuweka mikakati ya kupunguza udurusu wa mifumo na kuhakikisha mifumo yote ya TEHAMA, katika taasisi za umma inawasiliana na kubadilishana taarifa kupitia Mfumo Mkuu wa ubadilishanaji taarifa serikalini (GoVESB).

Kamati hiyo pia ilimchagua Connie Francis Mkurugenzi wa TEHAMA Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) kuwa Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo.